**CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)**
(Tanzania Teachers' Union – TTU)

P.O. Box 3077 DODOMA Fax: 262323452
Cable: WALIMU DODOMA Telephone: 262323451
E-mail: info@ttu.or.tz

Your Ref: .........................
Our Ref: AB.277/320/10/36 Date: 21/12/2022

Makatibu wa Mikoa,
**Chama cha Walimu Tanzania Bara.**

**YAH: TANGAZO LA KUJAZA NAFASI ZILIZO WAZI ZA VIONGOZI WANNE (4) WA CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT) MWAKA 2023.**

Tafadhali rejeeni mada tajwa hapo juu.

Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kinategemea kuwa na kikao cha dharura cha Mkutano Mkuu wa Taifa utakaofanyika mwezi Machi 2023 ajenda ni Uchaguzi wa kujaza nafasi nne za uongozi zizilizo wazi ngazi ya taifa ambazo ni Makamu wa Rais, Naibu Katibu Mkuu, Mweka Hazina wa Taifa na Mwenyekiti wa Kitengo cha Walimu Wanawake Taifa.

**A. NAFASI ZITAKAZOJAZWA:**

I. **Nafasi ya Makamu wa Rais wa Chama cha Walimu Tanzania** imebaki wazi baada ya aliyekuwepo kukosa sifa ya kuendelea kuwa katika nafasi hiyo kufuatia wajumbe kupiga kura ya kutokuwa na Imani naye.

**Sifa za wagombea:-**

- ✓ Awe mwanachama kamili wa CWT ambaye ametoa ada ya uanachama kwa kipindi cha mwaka mmoja mfululizo na kuendelea na sio kwa mkupuo.
- ✓ Awe Mwadilifu.
- ✓ Awe raia wa Tanzania.
- ✓ Mgombea atatakiwa kuungwa mkono na wanachama kamili kwa idadi ya wanachama thelathini (30).

II. **Nafasi ya Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania,** nafasi hiyo imebaki wazi kufuatia aliyekuwepo kuthibitishwa na Mkutano Mkuu Taifa kuwa Katibu Mkuu.

KATIBU MKUU
CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)
MAKAO MAKUU - DODOMA

**Sifa za wagombea:-**

- ✓ Awe mwanachama kamili wa CWT ambaye ametoa ada ya uanachama kwa kipindi cha mwaka mmoja mfululizo na kuendelea na siyo kwa mkupuo.
- ✓ Awe Mwadilifu.
- ✓ Awe raia wa Tanzania.
- ✓ Mgombea atatakiwa kuungwa mkono na wanachama kamili kwa idadi ya wanachama thelathini (30).

III. **Nafasi ya Mweka Hazina Taifa wa Chama cha Walimu Tanzania,** kufuatia aliyekuwepo kukosa sifa ya kuendelea na nafasi hiyo.

**Sifa ya wagombea:-**

- ✓ Awe mwanachama kamili wa CWT ambaye ametoa ada ya uanachama kwa kipindi cha mwaka mmoja mfululizo na kuendelea na siyo kwa mkupuo.
- ✓ Awe Mwadilifu.
- ✓ Awe raia wa Tanzania.
- ✓ Mgombea atatakiwa kuungwa mkono na wanachama kamili kwa idadi ya wanachama thelathini (30).

IV. **Nafasi ya Mwenyekiti wa Kitengo cha Walimu Wanawake Taifa wa Chama cha Walimu Tanzania,** kufuatia aliyekuwepo kukosa sifa za kuendelea kuwa katika nafasi hiyo.

**Sifa za wagombea:-**

- ✓ Awe mwanachama kamili wa CWT ambaye ametoa ada ya uanachama kwa kipindi cha mwaka mmoja mfululizo na kuendelea na siyo kwa mkupuo.
- ✓ Awe Mwadilifu.
- ✓ Awe raia wa Tanzania.
- ✓ Mgombea atatakiwa kuungwa mkono na wanachama kamili. kwa idadi ya wanachama thelathini (30).
- ✓ Awe mwanachama mwanamke.

## B. NYARAKA ZA KUAMBATANISHA:

Wagombea wote watatakiwa kurejesha fomu za mgombea zikiambatanishwa na nyaraka zifuatazo:-

- ❖ Salary Slip za mwezi Novemba 2022, Disemba 2022 na Januari 2023.
- ❖ Kivuli cha kitambulisho cha uanachama.

## C. WITO KWA WANACHAMA:

Chama kinatoa wito kwa wanachama wake kujitokeza kugombea nafasi hizo kwa wingi kwa kuwa ni haki yao kikatiba. Vilevile wanachama wanashauriwa



KATIBU MKUU
CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)
MAKAO MAKUU - DODOMA

kusoma kwa makini Katiba ya CWT Toleo la 6 la mwaka 2014, Kanuni za CWT toleo la 4 la mwaka 2015 na Kanuni za Uchaguzi za CWT toleo la 5 la mwaka 2015, pamoja na maelekezo ya tarehe ya kuchukua na kurejesha fomu. Wanachama wanakumbushwa kuwa muda wa kampeni utaanza siku ya mwisho ya kurudisha fomu hadi siku ya kupiga kura. Muda wa kupiga kura utakapoanza, hakuna mgombea atakayeruhusiwa kuendelea na kampeni.

Aidha kuanzia sasa Fomu za kuwania nafasi za uongozi zinapatikana ofisi za CWT Wilaya, ofisi za CWT Mikoa, Makao Makuu ya CWT jijini Dodoma, pamoja na kwenye tovuti ya Chama yaani (www.ttu.or.tz).

Mwisho wa kurejesha fomu ni tarehe 20 februari, 2023 saa 9:30 alasiri Makao Makuu ya CWT, Jijini Dodoma.

Wanachama wanatahadharishwa kuwa makini katika kipindi chote cha Uchaguzi na kujiepusha kabisa kutumia njia ya rushwa au kutoa ahadi zisizotekelezeka kutafuta kura. Yeyote atakayekiuka maadili ya Chama kuhusu Uchaguzi atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na **kunyang'anywa** ushindi ikiwa atakuwa ameshinda.

Chama kinapinga kwa nguvu zote matumizi ya Fedha, Rushwa na ushawishi, pamoja na kampeni za kulenga kuwachafua wagombea wengine. Licha ya kuwa rushwa ni adui wa haki, vivyo hivyo ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria za nchi kwa anayetoa na anayepokea.

Chama cha Walimu Tanzania kinawatakia kila la kheri kwa wale wote watakaojitokeza kuwania nafasi za uongozi ndani ya Chama.

Wenu kazini,

Maganga M. Japhet
**KATIBU MKUU – CWT**

KATIBU MKUU
CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)
MAKAO MAKUU - DODOMA

**NAKALA KWA:-**

1. Katibu Mkuu,
   Wizara ya kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu,
   Mji wa Serikali - Mtumba,
   S. LP 2890.
   **DODOMA.**

2. Mkurugenzi Mkuu,
   Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa,
   S.L.P. 1291,
   **411101 DODOMA.**

3. Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri.
   S.L.P 2890,
   **DODOMA.**